

SHULE YA SEKONDARI NYAMTINGA

S.L.P 119

SHIRATI-RORYA

TAREHE.....

KUMB NA: NYAM. SS/VOL.01/2021

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAMTINGA, WILAYA RORYA, MKOA WA MARA MWAKA 2020.

1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) - 2021 katika shule ya Sekondari Nyamtinga. Shule ipo umbali wa km 30 Magharibi ya Halmashauri ya Wilaya ya **RORYA**.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11 Januari 2021** na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11 Januari 2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **19 Januari 2021**, ndani ya siku saba (7).

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(a) Sare za shule

- Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi.
- Suruali mbili (2), moja ya rangi ya **Bluu Bahari** na moja rangi ya **Dark Green** kwa wavulana, yenye malinda mawili na isiyokuwa mtindo wa modo. Sare ya **Blue Bahari** itavaliwa siku za **Jumatatu** hadi **Jumatano** na sare ya **Dark Green** itavaliwa **Alhamisi** na **Ijmaa**. Suruali lazima zivaliwe na mikanda ya rangi nyeusi.
- Sketi mbili (2), moja ya rangi ya **Bluu Bahari** na moja rangi ya **Dark Green** kwa wasichana. Sketi ziwe na malinda 8 au yasiyozidi 19. Kitambaa kiwe kizito na sio tetron, Sketi fupi na vimini ni marufuku. Sare ya **Blue Bahari** itavaliwa siku za **Jumatatu** hadi **Jumatano** na sare ya **Dark Green** itavaliwa **Alhamisi** na **Ijmaa**.
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba ila visiwe mtindo wa buti. Raba au simple haziruhusiwi.
- Soksi ndefu nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
- Sweta ya rangi ya **Bluu** kwa wavulana na wasichana.

(b) Sare za michezo.

- Raba
- T-shirt ya blue

- Bukta kwa wavulana na traki kwa wasichana.

3.0 MAMBO MENGINE

- Kalamu, madaftari 10 (countre books quire 2)
- Mkebe wa hisabati (mathematical set)

4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1975 na kama ilivorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia Miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya waziri mkuu (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule.
5. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
6. Kuvaa sare ya shule wakati wote ukiwa shuleni siku za shule.
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
8. Kutunza mali za umma.

4.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
5. Kupigana au kupigwa
6. Kuharibu kwa makusudi mali za umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito au kupata pimba
9. Kugoma au kuchochea na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
10. Kuoja au kuolewa
11. Kukataa kufanya adhabu

12. Kuwa na simu ya mkononi shuleni

4.3 MAELEZO MUHIMU.

Unatakiwa wewe mzazi/mlezi wa mwanafunzi uwe umesoma na kuelewa vema sheria za shule na kanuni zake na kujaza fomu hii na kukabidhi siku mwanafunzi atakapokuwa anaripoti shuleni. Unatakiwa kumleta mwenyewe mwanao shuleni siku ya kufungua shule tarehe **11 Januari 2021** na mahitaji yote ya shule bila kukosa.

SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi..... (jina kamili) ambaye umechaguliwa kujiunga na masomo kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Nyamtinga kwa mwaka wa masomo 2021, naahidi kuwa nimesoma na kuelewa kanuni na sheria za shule na nimekubali kufuata sheria na kanuni hizo zote.

JINA LA MWANAFUNZI..... *SAHIHI*.....

SEHEMU YA MZAZI

Mimi (mzazi/mlezi) wa (Jina la mwanafunzi), naahidi kumlea mwanangu kulingana na sheria na kanuni za shule na mwanangu amekubali kufuata sheria na kanuni hizo. Pia naahidi kushirikiana na walimu kumlea kwa mujibu wa sheria na kanuni za shule.

JINA (mzazi/mlezi)..... *SAHIHI*.....

.....


SAMWEL PAMBA

MKUU WA SHULE

**HEAD MASTER
NYAMTINGA SCHOOL
P.O. BOX 19
SHIRATI-RURYA**